



TAARIFA KWA UMMA

THAMANI YA SHILINGI

Benki Kuu inapenda kutoa taarifa kuwa, hadi kufungwa kwa soko la jumla la fedha za kigeni linaloendeshwa na Benki Kuu leo jioni tarehe 3 Novemba 2017, shillingi ya Tanzania ilikuwa inauzwa kati ya shilingi 2,246.50 na shilingi 2,247.60 kwa dola ya Marekani.

Hata hivyo, majira ya saa 12:30 jioni leo, takwimu za Bloomberg zilionyesha thamani ya shilingi kushuka hadi kufikia shilingi 2,481.83 kwa dola ya Marekani—**taarifa ambayo siyo sahihi**. Baada ya mawasiliano na Blomberg ilionekana kuwa baadhi ya wachangiaji waliingiza takwimu zisizo sahihi na hivyo marekebisho yakaanza kufanyika.

Benki Kuu inapenda kufahamisha umma kuwa kuna kuna hazina ya kutosha ya fedha za kigeni na hakuna sababu ya taharuki.

IMETOLEWA NA IDARA YA UHUSIANO NA ITIFAKI

03 NOVEMBA 2017.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na: akngwinamila@bot.go.tz